**Learning by Ear 2009**

# Media & Information

**Author: Hope Azeda**

**Redaktion: Ludger Schadomsky**

**Kisuaheli Translation:Eric Ponda**

**EPISODE 5**

| | |
|---|---|
| *CHARACTERS* | |
| Announcer: | Male/female |
| "Young Junior" | Male, 15 years old |
| "Sister P." | Female, 16 years old |
| "Charlie" | Male, 18 years old |
| Director of Institute | Adult male |

**INTRO**

Hujambo na karibu kwa makala nyingine ya Learning By Ear tukizungumzia uandishi na vyombo vya Habari. Muda unazidi kuyoyoma huku matumaini yakizidi kudidimia kwa wanahabari wetu chipukizi kuhusiana na mradi wao wa

kujenga kitu cha cha redio ya kijamii, baada ya kubainisha kuwa si kazi rahisi kuanzisha kituo hicho. Ezra amewashauri kwamba wanahitaji kima cha Yuro 7,000 kuanzisha kituo hicho huku wanahabari hao wakiwa ndio mwanzo hawajapata mafunzo maalum ya uandishi wa habari. Je yote yatakuwa pingamizi ya kufanikisha azma yao .Ungana nasi usikie yatakayoenelea  katika makala hii ifuatayo, tukianzia katika kituo cha vijana.

**SCENE ONE**

**At the youth centre, the place is as busy as it was in episode one, with some youths are playing football; the karate team can also be heard in the distance doing their exercises.**

**Sfx  Fast footsteps on the floor, Door opens.**

2. **Sister P:** Young J,  Charlie yuko wapi? Bado hajafika?

3. **Young J:** Labda  tumuangalia. Mwelekezi anasema yuko hapa kituoni

4. **Sister P:** Twende tumtafute basi . Tuna mambo mengi sana ya kufanya , kwani sitapumzika hadi nitakapo hakikisha  kituo cha Dot.Com kiko hewani kupeperusha matangazo.

**SFX Door shuts and footsteps heard on the floor.**

**6. Sister P:** Lakini kama Charlie hayupo hapa chumba cha mazoezi, anawezakuwa yuko wapi? Katika ukumbi wa mazoezi ya Karate? Pengine Gym, uwanja wa kandanda au anaweza kuwa wapi?

**7. Young J:** Beskeli yake iko pale. Kwa hivyo ni lazima awe yumo katika jengo lile la ofisi.

**8. Sister P:** Sasa amekwenda kufanya nini kule?Mungu wangu kwani Charlie ameanza biashara ya kuoka mikate? Na lile boksi analobeba nyuma ya Beskeli yake lina nini ?

**9. Young J:** Nani ajuae?

**10. Charlie:** (**From a distance).** Young J, Nimemiliza shughuli zangu hapa, njooni upesi nina habari njema!.

**11. Sister P:** Umekuwa ukifanya nini kule?. Tumekutafuta kila mahali kama mototo aliyetoweka.

**12. Charlie:** (**Approaching).** Nimekwenda ofisini kuulizia uwezekano wa kupata chumba kidogo tu.

**13. Young J:** Usiseme unapendekeza kutumia chumba kile kidogo kama studio. Ni chumba kidogo sana,hakina hata madirisha,yaani namaanisha kwa kweli chumba hiki…..

**14.** hakiwezi kutumika kama studio za redio Dot.Com,

**15. Sister P:** Kusema kweli , Charlie, hutarajii tutumie chumba kile …

**16. Charlie:** Eh hapana nitaka kutumia chumba kile kuweka baadhi ya vifaa tu wakati tutakapovipata.Tayari nimepata mixer kuu kuu kutoka Dubai.

**17. Sister P:** Hehehe,hizo ni habari njema! . Nani aliyekupa Charlie? Na bado ni nzuri inafanya kazi?

**18. Charlie:** Ndio, hebu njoni muione. Na si ghali!. Anayeniuzia anasema kuwa tunaweza kumlipa kiasi cha euro 600 pekee.

**19. Sister P:** Hebu kidogo. Umesema euro 600? Nilifikiri aimekupa kama zawadi au umesahau ulivyotwambia

**20. Charlie:** Hapana, tunapaswa kuilipia!.

**21. Sister P:** Sasa wenzangu tayari tumeanza shughuli zetu lakini lazima tuwe waangalifu kama Ezra alivyotushauri. Lazima tujitolee na kuzingatia malengo yetu.

**22. Young J:** Sawa Malikia wa Dot Com. Lazima tuheshimu maoni yako malikia!

**23. Sister P:** Sawa mheshimiwa , acha huo upuzi jina langu Sister P. Napendekeza zile pesa kidogo tulizo nazo kwenye akaunti ya Dot.Com tutumie kulipia kozi ya

uandishi wa habari, kuandika mapenekezo na kujaribu kupata pesa na wafadhili wengine zaidi.Pia kuandaa ziara ni muhimu ikiwezekana

**24. Charlie** …Na kuhusu mixer?

**25. Sister P:** Unaweza kuirudisha kwa aliyekupa na umwambie asante. Kwa sasa tunapaswa kuelekea chuoni mjini, kama tulivyoshauriwa na Ezra ili tuone ni kozi gani tunaweza kuchukua na kujua gharama zake pia.Iwapo tunapaswa kufanikisha mradi huu, mafunzo ni muhimu au unasemaje Young J?

## SCENE TWO

**At the City Institute of Journalism and Tourism. The place is relatively calm.**

**SFX of doors opening and closing and people walking in corridors. In the far distance a film director is heard giving instructions to the crew: "*Action and cut*"**

**27. Sister P:** Wenzangu,hapa ni chuoni kweli?

**28. Young J:** Sasa hilo ni swali gani unauliza Sister P? Ama huoni maandishi "THE CITY INSTITUTE OF JOURNALISM" yaani "Chuo cha uandishi jijini" yaani ?

**29. Charlie:** Nimechanganyikiwa ,bango hili linasema ni chuo cha mafunzo ya uandishi wa habari, lakini hapa

kando kidogo kuna bango linaloelezea nafasi za kazi katika taaluma ya upishi na utalii.

**30. Sister p:** Kweli inashangaza!. hiki ni chuo cha uandishi wa habari,upishi au utalii?

**31. Young J:** Wewe huelewi .Hili bango linasema kuwa chuo hiki kimepanuliwa shughuli zake na sasa kinatoa mafunzo ya utalii mbali na uandishi wa habari.

**32. Charlie:** Hapa kuna kila fursa ya kufanikisha malengo yako maishani. Huwezi kutoka chuoni hapa bila ya cheti cha kuhitimu. Ukianguka mtihani katika sekta ya uandishi unaweza kusomea upishi..ukianguka mtihani wa kuhusu upishi unaweza kusomea masuala ya utalii. …! na ukianguka sekta zote hizo basi umeanguka mtihani maishani…...

| |
|---|
| **SFX A film director heard saying "*Action*".** |

**34. Charlie:** Hebu tuangalie hapa, wanatayarisha filamu. Tunaweza kuona dakika chache tu labda tunaweza kujiunga nao siku moja?

**35. Sister P:** Sasa tumeanza kuwa kigeugeu. Tumekubaliana kuzingatia suala moja, kwanza twende kumuona mkufunzi mkuu wa taasisi kisha baadaye tunaweza kuzurura huku na huko.

**36. Charlie:** Sawa nakubaliana nawe!

**37. Sister P:** Sawa umeshindwa.

**SFX Knocking on the door.**

**39. Director** Piteni ndani mlango uko wazi!.

**SFX Door opening**

**41. Director** Karibuni mkae.

**SFX Door closing and tables scratching the floor**

**43. Director:** Karibuni katika taaisisi hii ya uandishi wa habari,utalii na masuala ya nupishi. Ehe nawasaidie na nini ?

**44. Sister P:** Sisi ni wanachama wa kundi la vijana la DCC.

**45. Director:** Nini maana ya DCC? Idara inayoshughulikia masuala ya watoto au vipi?

**46. Young J:** Hapana.. hapana DCC inamaanisha Dot.Com Club.

**47. Director:** **(Laughs)** Klabu ya silaha za maangamizi au vipi? Sawa sasa niwasaidie na nini ?

**48. Charlie:** Tunampango wa kuanzisha kituo cha redio ya jamii, na msingi tunashauriwa tupata mafunzo ya uandishi wa habari

**49. Director:** Sawa mumefika. Lini munatarajia kuanzisha kituo hicho na ni mafunzo ya aina gani mnayohitaji ?

**50. Sister P:** Kwa kweli hatujui lolote kuhusu masuala ya uandishi au mafunzo yanayotolewa na chuo hiki. Labda pengine tukuwambie utaratibu kisha ukatushauri zaidi..

**51. Director**: Sawa basi tunaweza kuanza.

**52. Charlie:** Tunataka kuanzisha kituo ambacho kitawalenga zaidi vijana,kikiwa na wingi wa burudani, lakini pia vipindi vya kuelimisha katika msuala ya Afya, Biashara,siasa Kilimo na kadhalika.

**53. Young J:** Nadhani hatukukanganyi Bw mkurugenzi.

**54. Director:** Hapana hapana…Naelewa munachotaka. Je mumepata mafunzo yoyote hapo mbeleni?

**55. All:** La..!.

**56. Director:** Tuko na kozi za aina mbali mbali. Kuna kozi ya miaka miwili na hatimaye mwanafunzi kufuzu na shahada ya Diploma.

**57. Charlie:** Inachukua muda mrefu?.

**58. Director:** Pia tuna kozi ya miezi sita ambapo mwanafunzi anayehitimu hupata cheti..

**59. Sister P:** Ni kozi nzuri lakini bado inachukua muda mrefu.

60. **Director:** Pia tuna kozi ya wiki mbili ambapo mwanafunzi anapofuzu hupewa cheti.

61. **Young J:** Hii ndio kozi inayotufaa.Mwanafunzi husomea nini katika kozi hii ya wiki mbili?

62. **Director.** Kozi hii inatoa mafunzo ya kimsingi ya uandishi wa habari. Mwanafunzi hupata mafunzo kuhusu utayarishaji vipindi,uhariri,usimamizi na uandishi wa habari. Pia tunawapa ushauri na vidokezo wanafunzi wanaotaka kuanzisha vituo vya redio vya jamii.

63. **Sister P:** (E**xcited).** Nadhani sasa tumepata tunachohitaji.Tujiunge mara moja. Na karo ni kiasi gani?

64. **Director**: Nitamupa maelezo yote kuhusu kozi hizi.

65. **Charlie:** Munatoa mafunzo kuhusu masuala ya Televisheni? Tuliwaona watu wakitayarisha filamu hapo nje.

66. **Director:** Kwa wakati huu hatuna mafunzo ya Televisheni. Watu hao muliowaona hapo nje ni wanafunzi wa idara ya uandishi wa habari wanaotayarisha mchezo wa kuigiza.Nimewapa idhini ya kutumia eneo hilo.

67. **Charlie:** Tunaweza kwenda kuona kinachoendelea ?

**68. Director:** Siwezi kuwapa idhini hiyo,labda mumuombe ruhusia mkurugenzi wa wa idara ya filamu.

**69 Sister P** Sawa nadhani sasa wanapumzika. Tunaweza kuzungumza na mkurugenzi kama atakubali kutupa ushauri wowote..

**70. Charlie/Y.J:** Twendeni basi!

**END EPISODE.**

## *OUTRO*

Naam hadi hapo tunafika mwisho mwa makala haya ya leo ya Learning By Ear kuhusu habari na Vyombo vya Habari. Natumai umefurahia kipindi hiki na bila shaka utaungana nasi wakati mwengine kufahamu zaidi kuhusu juhudi zinazofanywa na Young J na wenzake katika kutafuta fedha za kufadhili mradi wao. Pia ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa dw-world.de/lbe.

Ukiwa na maoni pia usisite kututumia na hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.